

HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBITI

MUHTASARI WA KIKAO CHA WAKUU WA IDARA NA VITENGO (CMT)

KWENDA KWA: WAKUU WA IDARA NA VITENGO

KUTOKA KWA: AFISA UTUMISHI NA UTAWALA (W)

Kumb Na: AJ.81/177/321/106

YAH: MAMBO YA KUFANYIA KAZI KUFUATIA KIKAO CHA CMT CHA TAREHE 16/02/2022.

MAHUDHURIO:

A: WATAALAMU WALIOHUDHURIA: KIKAO CHA CMT CHA TAREHE 16/02/2022.

- | | |
|--------------------------|-------------------------------|
| 1. Bw. Denis E. Kitali | -Kaimu Mkurugenzi Mtendaji |
| 2. Bw. Sudi S. Khassim | - Kaimu Afisa Utumishi |
| 3. DR. Elizabeth Oming'o | -Mganga Mkuu (W) |
| 4. Bi. Rehema Isaay | - Mwekahazina (W) |
| 5. Bw. Tumainiel Kamnde | -Afisa Manunuzi (W) |
| 6. Bw. Rudrick Charles | -Afisa Mipango (W) |
| 7. Bw. Anthony Nyange | -Afisa Maendeleo ya Jamii(W) |
| 8. Bw.Mfaume S.Jeta | -Afisa TEHAMA |
| 9. Bw.Bwenda I. Bainga | -AfisaKilimo, Umwagiliaji(W) |
| 10. Bw. Swalehe Njoma | -Mwanasheria (W) |
| 11. Eng.kassim Mponda | -Kaimu Mhandisi Ujenzi(W) |
| 12. Bw.Laban Kitule | -Kaimu Afisa Mazingira |
| 13. Bw.Damas Kimaro | -Kaimu Afisa Elimu Msingi |
| 14. Bw. Jamal Saidi | -Mratibu TASAF (W) |
| 15. Bw. Hamadi Mgaluli | -Kaimu Afisa Nyuki (W) |
| 16. Bw.Justus Lugome | - Kaimu Afisa Elimu Sekondari |

B. WASIO HUDHURIA KWA TAARIFA.

- | | |
|--------------------------|--------------------------------------|
| 1. Bw. Mohamed I. Mavura | -Mkurugenzi Mtendaji (W)-Kwa taarifa |
|--------------------------|--------------------------------------|

C. SEKRETARIET.

- | | |
|--------------------|---------------------|
| 1. Bw. Mao Kasanga | -Mwandishi wa Vikao |
| 2. Bi. Raya Mlawa | -Mwandishi wa Vikao |

AGENDA NA. 01: KUFUNGUA KIKAO

Makamu Mwenyekiti alikaribisha Wajumbe kikaoni, alieleza kuwa kikao cha Menejimenti cha Kila Jumatano Ambacho pia kitapitia taarifa zinazoingia kwenye Kikao cha Kamati ya Fedha Uongozi na Mipango pamoja na Utekelezaji wa Kazi za wiki hivyo aliomba wajumbe kuwa makini katika kujadili taarifa zinazowasilishwa.

Baada ya kusema hayo alifungua kikao saa 08:30 Asubuhi.

AGENDA NA. 02: KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO.

Jumla ya agenda Tisa (9) ziliwasilishwa kikaoni ili zijadiliwe nazo ni;

1. Kufungua Kikao.
2. Kuridhia Agenda.
3. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa tarehe 16/02/2022.
4. Yatokanayo na kikao cha CMT cha tarehe 16/02/2022
5. Taarifa ya Mapato ya Wiki kuanzia tarehe 07/02/2022 Hadi 13/02/2022
6. Taarifa ya DEFAULTER's
7. Taarifa ya Mapokezi ya fedha kiasi cha **Tshs. 300,000,000.00** kwaajili ya Ujenzi wa Jengo la dharula katika Hospitali ya Wilaya ya Kibiti.
8. Taarifa za Utekelezaji wa Kazi za Idara.
9. Kufunga kikao.

Baada ya agenda hizo kupitiwa Wajumbe wote kwa pamoja waliridhia agenda zote Tisa (9) Kujadiliwa.

AGENDA NA 07: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSHS. 300,000,000.00 KWAAJILI YA UJENZI WA JENGO LA DHARULA KATIKA HOSPITALI YA WILAYA YA KIBITI.

Kwa idhini ya Mwenyekiti Mweka hazina aliwasilisha taarifa ya Mapokezi ya fedha kama ifuatavyo;-

Ilielezwa kuwa Halmashauri imepokea kiasi cha fedha **Tshs. 300,000,000.00** kutoka Serikali kuu ikiwa ni Fedha za UVIKO-19, ilielezwa kuwa fedha hizo zimeingia tarehe , 11/01/2022

Ilielezwa kuwa fedha hizo ni kwaajili ya Ujenzi wa jengo la dharula katika hospitali ya Wilaya ya Kibiti

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa Menejimenti ilisisitiza barua ya taarifa ya mapokezi ya fedha ipelekwe Kwa mtendaji Kata pamoja na Mhe. Diwani wa Kata ya Mtawanya ili wananchi wapatiwe taarifa, sambamba na maandalizi ya Uundwaji wa Kamati na utangazaji wa Zabuni vyote vianze mapema ili kwenda na muda.

Baada ya Mjadala huo Wajumbe wote kwa pamoja waliridhia na kupitisha

AGENDA NA 09: KUFUNGA KIKAO.

Makamu Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe kwa miachango yao na kuisitiza yaliyoagizwa yakafanyiwe kazi. Baada ya maelezo hayo alifunga kikao saa 06:00 Mchana.


MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA;


.....

SAINI YA MWENYEKITI


.....

JINA LA MWENYEKITI


.....

TAREHE


.....

SAINI YA KATIBU


.....

JINA LA KATIBU


.....

TAREHE